BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukuwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000

info@zanzibarassembly.go.tz

# MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Spika, naomba nianze Kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, tukiwemo sisi waja wake. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia Uzima, Afya njema na uwezo wa kukutana hapa leo ili kuweza kuendelea na kutekeleza majukumu yetu ya Kikatiba ya kuwatumikia Wananchi wetu kwa faida ya Nchi na wananchi wetu tunaowawakilisha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa nimesimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama inavyoelekeza Kanuni ya 109(15) ya Baraza lako Tukufu, Toleo la mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee na kwa niaba ya Kamati yangu adhimu napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Salha Mohamed Mwinjuma kwa kupata uteuzi siku ya tarehe 27 Januari, 2024 kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, na Maendeleo ya Makaazi. Uteuzi huo umeongeza nafasi za Wakinamama na kukuza usawa wa jinsia katika ngazi ya uongozi.

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Salha alikuwa Mtendaji mahiri, mwenye maono na mweledi katika utekelezaji wa kazi za Kamati, Kwa kweli busara za Rais wa Zanzibar na

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi zimeenda kwa mtu sahihi na kwa wakati sahihi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inamuahidi kwamba itampatia kila aina ya ushirikiano na kumjulisha kwamba asitupe jongoo na mti wake. Aidha, Kamati yetu inampongeza Mheshimiwa Jamal Kassim Ali kwa kupata uteuzi wa Mheshimiwa Spika siku ya tarehe 29 Januari, 2024 kumleta katika Kamati yetu kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya PAC. Kamati haina kubwa la kumwambia isipokuwa akaribie vyema. Kamati inategemea kunufaika mengi kutokana na uzoefu wake mkubwa alionao hususan katika masuala ya uchambuzi wa matumizi wa mapato ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Kamati ya PAC ilizifanyia kazi Ripoti tano kama zifuatazo:-

1. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022;
2. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022;
3. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022;
4. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022; na
5. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi

wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa niaba ya Kamati ya PAC, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani kwa Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika kazi za Kamati yetu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** kiujumla. Kamati ya PAC imegundua kuwa Wizara na Taasisi za Serikali zimekuwa zikirekebisha dosari za kiutendaji zinazobainishwa na vyombo vya Uchunguzi na Udhibiti wa Hesabu za Serikali ikiwemo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Kamati ya PAC. Hivyo, kwa kiasi kikubwa kiwango cha nidhamu ya matumizi ya rasilimali za umma katika Serikali zimeimarika.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya juhudi hizo, Kamati ya PAC imebaini kuwa bado kuna maeneo kadhaa ambayo Serikali inahitaji kuongeza jitihada za kuyafanyia kazi ili utekelezaji wa mipango ya Serikali ufuate Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo zikiwemo zinazosimamia masuala ya fedha na ununuzi katika utendaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Katika ukaguzi uliofanywa na Kamati yetu, mambo yafuatayo yalibainika:

1. **Kutounganishwa kwa Mifumo ya ukusanyaji Mapato ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

**Mheshimiwa Spika,** licha ya juhudi kubwa ambazo Mamlaka ya Mapato Zanzibar inazichukuwa kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa taarifa sahihi za wasafiri kupitia Bandarini na Viwanja vya Ndege. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kuwa kumekuwa na changamoto zinazorudisha nyuma utekelezaji wake kwa vile bado hakujakuwa na uungwanishwaji wa mifumo inayotoa taarifa sahihi na za pamoja hususan kwa Wageni na Watalii wanaoingia na kutoka Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** hali hiyo hupelekea kutofautiana kwa taarifa zilizopo katika Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Kamisheni ya Utalii na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar. Aidha, huikosesha mapato Serikali kwa vile kuna uwezekano mkubwa wa kutoa mwanya kwa watu wachache kujinufaisha na ukusanyaji wa mapato hayo kutokana na kutokuingizwa mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar tayari imeshaandaa Mfumo mpya wa GADIS utakautumika kukusanya taarifa za Wageni wanaoingia na kutoka Zanzibar kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ambao unategemewa kuwa muarubaini katika upatikanaji wa taarifa sahihi katika eneo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imegundua kuwa tayari Mamlaka ya Mapato Zanzibar na Kamisheni ya Utalii zimeshakubaliana juu ya uunganishwaji wa mifumo yao ili taarifa za Watalii waliopo Zanzibar zinapatikana kwa usahihi wake na kukuza ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka. Kuwepo kwa muunganiko wa mifumo hiyo kutaisaidia Serikali sio tu kujua takwimu za Watalii waliofika na kulala katika Mahoteli ya Zanzibar bali utatatua changamoto za masuala ya kiusalama wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu uliopo katika uunganishwaji wa mifumo hiyo, Kamati ya PAC inaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar kuhakikisha inaendeleza juhudi za kuunganisha mfumo wao na mifumo ya Taasisi nyengine ili taarifa sahihi za Wageni wanaoingia na kutoka Zanzibar ziweze kupatikana. Aidha, Serikali kupitia Wizara Utalii na Mambo ya Kale ichukue juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba Mifumo ya Kampuni za masuala ya Utalii hususan za Watu binafsi zinaunganishwa katika Mfumo wa ZRA ili taarifa za makusanyo yao ziweze kupatikana na kutumika katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutathmini utendaji wa Mamlaka zinazohusika na upakiaji na

ushushaji wa mafuta Zanzibar. Kamati ya PAC imebaini kuwa Mamlaka husika zinaendelea kufanya kazi zao kwa 'manual' bila ya kutumia mfumo mmoja wa kielektroniki na kupelekea kuwepo na shaka za kiutendaji na kupunguza ufanisi katika ukusanyaji wa Mapato kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Taaisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) pamoja na Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) kila moja kufanyakazi peke yake.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) tayari imeshaishauri Serikali juu ya uwepo wa Mfumo mmoja utakaoziunganisha Taasisi zote tano na kuziwezesha kufanya kazi kwa pamoja jambo ambalo litasaidia kupatikana kwa taarifa sahihi zitakazotumika kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uungwanishwaji wa mfumo wa Mapato wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZIDRAS) na mfumo wa usajili wa kodi za Ardhi unaotumiwa na Kamisheni ya Ardhi Zanzibar, Kamati yetu imegundua kuwa kuna changamoto ya upatikanaji wa taarifa za mapato yatokanayo na kodi ya ardhi. Hili limetokana na kutounganishwa kwa mifumo hiyo na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutatua changamoto hiyo, ZRA imefanya mawasiliano na Kamisheni ya Ardhi kupitia barua ya tarehe 6 Julai, 2023 yenye kumbukumbu nambari ZRA/BC.178/298/01/32 bila kupata majibu yoyote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC iliiandikia barua Kamisheni ya Ardhi siku ya tarehe 14/2/2024 yenye kumbukumbu nambari CE.81/204/02/45 na kubaini kwamba Sheria ya Kamisheni ya Ardhi nambari 6 ya mwaka 2015 katika kifungu cha 22(3)(b) imeainisha kuwa tozo pamoja na kodi za ukodishwaji wa ardhi itakayokusanywa na Kamisheni itakuwa ni chanzo chao cha mapato. Hata hivyo, Sheria mpya ya Mamlaka ya Mapato

Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2022 katika kifungu chake cha 7, kimeeleza usimamizi wa sheria zisizokuwa za kodi zisimamiwe na Mamlaka ya Mapato baada ya Mawaziri wa Taasisi zinazosimamia sheria hizo kukubaliana.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC inautaka uongozi wa ZRA na Kamisheni ya Ardhi uhakikishe unaunganisha mifumo yao ya ukusanyaji mapato ya kodi ya ardhi ili kuiwezesha Serikali kupata mapato halisi kulingana na taarifa za ukodishwaji ziliopo.

**Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kinakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa Mtandao (internet) ya kuwawezesha Wanafunzi na Walimu wao kujifunza na kusomesha kwa urahisi. Hali hiyo imesababishwa na kiwango kidogo na chenye 'speed' ndogo yenye bandwith 200 kutoka Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA). Katika kutatua changamoto hiyo, SUZA imefanya mawasiliano na Tanzania Education Research Network (TERNET) inayotoa huduma za mtandao katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti wenye 'speed' kubwa na kwa bei nafuu.

**Mheshimiwa Spika,** iwapo SUZA watafanikiwa kujinga na TERNET watafaidika na huduma tofauti wanazozipata Vyuo vyengine Duniani zikiwemo:

1. Upatikanaji wa 'internet' yenye nguvu zaidi kwa bei nafuu;
2. Upatikanaji wa huduma ya Walimu na Wanafunzi kufundisha na kujisomea nje ya maeneo yao ya huduma kwa wepesi zaidi;
3. Upatikanaji wa msaada wa kiufundi katika masuala ya TEHAMA; na
4. Kuongeza nguvu 'speed' ya mtandao bila ya kuongeza gharama za ununuzi au kubadilisha masharti ya Mkataba husika.

**Mheshimiwa Spika,** ili SUZA iweze kunufaika na huduma za Taasisi hiyo, TERNET wanalazimika kuomba ZICTIA ili kupatiwa ruhusa ya matumizi ya Mkongo wa Taifa.

Hata hivyo, ZICTIA imeshindwa kutoa ruhusa hiyo kwani wanaiangalia TERNET kama ni Taasisi ya kibiashara kama yalivyo Makampuni ya Simu na sio kama ni Taasisi ya kuwezesha utoaji wa huduma katika Vyuo Vikuu na ufanyaji wa Tafiti tofauti jambo ambalo litawasaidia Wanafunzi na Walimu kujifunza ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu ilifanya ziara katika Ofisi za Taasisi hizo ziliopo katika Chuo Kikuu Dar es Salaam na kubaini kwamba kwa vile Taasisi hiyo ina uwezo mkubwa wa kutoa huduma hizo ambapo kama wataruhusiwa kuleta huduma ya Mtandao, SUZA wataweza kupata hadi Bandwith 1,000 badala ya 500 wanazotarajia kuzipata kutoa ZICTIA.

**Mheshimiwa Spika,** ili kufikisha huduma za mtandao kufikia SUZA. TERNET wamechukuwa jitihada kadhaa za kuwasiliana na ZICTIA bila mafanikio. Kubwa zaidi, TERNET wamekutana na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kuzungumzia suala hilo bila ya mafanikio yoyote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC ilibaini kuwa hoja hiyo inahitaji kufuatiliwa zaidi kwa kupata majibu ya upande mwengine wa Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) ili iweze kupata ukweli na usahihi wa majibu yaliyotolewa na kuweza kuishauri ipasavyo Serikali.

**2. Upatikanaji mdogo wa fedha za matumizi kinyume na Bajeti iliyoidhinishwa**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ya PAC imebaini kwamba kuna Taasisi nyingi ambazo hazikuingiziwa fedha ipasavyo ukilinganisha na Bajeti iliyoidhinishwa na Baraza lako. Hali hiyo hupelekea baadhi ya shughuli walizojipangia kutekeleza hushindwa kukamilika kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa.

Kamati imelibaini hilo ilipotembelea Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ambao wamepatiwa asilimia 34.9 na asilimia 35 kwa Wakala wa Majengo ya makadirio yao.

Kwa msingi huo, kuwepo kwa changamoto hii kwa kiasi hicho kunapelekea kushindwa kutekeleza baadhi ya huduma zao muhimu za Afisi zao. Kamati inaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuziingizia Taasisi hizo fedha kwa mujibu wa Bajeti iliyoidhinishwa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

3. **Kuwepo kwa malimbikizo ya madeni ya Mishahara kwa Wafanyakazi na kwa Watoa huduma.**

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa jambo la msingi ambalo Serikali inatakiwa kulifanyia kazi kwa uharaka wake ni ulipwaji wa maslahi ya Wafanyakazi na Watoa huduma. Kamati imebaini kuwa bado kuna Taasisi za Serikali zinakabiliwa na madeni ya Wafanyakazi pamoja na Watoa huduma mbali mbali. Miongoni mwa Taasisi hizo ni pamoja na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa malimbikizo ya madeni ya mishahara kwa Wafanyakazi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali waliorudi masomoni kwa vipindi tofauti kuanzia 2018, Kamati imechukua juhudi ya kufuatilia changamoto hiyo kwa kufanya kikao cha pamoja na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Wizara inayohusiana na Utumishi wa Umma na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali siku ya tarehe 16 Febuari, 2024 na kukubaliana kwamba fedha halisi zinazopaswa kulipwa kwa Wafanyakazi 20 ni shilingi 53,710,880 badala ya shilingi 60,943,129 kwa vile kuna fedha ya malipo ya ZSSF ndani yake ambapo kila Taasisi itekeleze wajibu wake kuhakikisha madeni hayo yanalipwa kwa Wafanyakazi husika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa vile deni hilo ni la muda mrefu na limeshachukua takriban miaka sita iliyopita lakini bado halijalipwa. Kamati imeagiza kwamba ifikapo tarehe 28 Febuari, 2024 Taasisi hizo zikutane tena na Kamati kuelezea hatua ya utekelezaji wake.

4. **Madeni yanayodaiwa na Taasisi za Serikali ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imebaini kuwa baadhi ya Taasisi za Serikali zinashindwa kusimamia ipasavyo madeni yanayotokana na utoaji wa huduma tofauti. Hali hiyo hupelekea kukosekana kwa mapato ya Serikali na kurudisha nyuma utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo. Aidha, baadhi ya Taasisi za Serikali hususan Mashirika hushindwa kuwasilisha gawio lililopangwa na Serikali kwa wakati na kurudisha nyuma maendeleo ya ufikishaji wa huduma za msingi kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa Taasisi ambazo zinadai hususan kwa Taasisi za Serikali ni pamoja na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ambapo wakati wa ukaguzi walidai shilingi 59,190,000 na kulipwa shilingi, 920,000 na kudai shilingi 49,230,000, madeni ya shilingi bilioni 2,690,294,721.80 na dola za Kimarekani Milioni 3,760,749.39 kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar yanayohusiana na tathmini za kodi za muda mrefu pamoja na shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni 11,792,372,565.06 kwa Shirika la Bandari Zanzibar wakati Wakala wa Majengo unadai jumla ya shilingi 568,556,600 kwa upande wa Unguja tu za ukodishaji mali zake na utoaji huduma ya ushauri elekezi kwa Taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Shirika la Bandari Zanzibar, Kamati imebaini Shirika limeshindwa kusimamia ipasavyo ulipwaji wa deni la muda mrefu la shilingi 66,960,000 linalotokana na ukodishwaji wa nyumba ya Shirika iliopo eneo la Shangani ambapo hadi Kamati inapokea majibu ya hoja hii bado deni hilo halijalipwa licha ya Shirika kuchukua hatua kadhaa kufuatilia deni bila ya mafanikio ikiwemo kumuandikia barua za ukumbusho Mkodishwaji na ufanyaji wa vikao vya pamoja kuhusiana na ulipwaji wa deni hilo. Hata hivyo, Kamati ilitaka kupatiwa nakala ya Mkataba wa ukodishwaji pamoja na barua za ukumbusho lakini hakuna kielelezo chochote kilichowasilishwa mbele ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kutokuwepo kwa muhusika ndani ya nchi pamoja na Kamati kutopata muda wa kulifuatilia suala hilo kwa upana wake kwa vile muda wa

kuwasilisha ripoti hii ulikuwa umefika. Hata hivyo, Kamati imeazimia kumwita Mkodishwaji huyo ili kupata fursa ya kukaa nae na kujua ukweli ulivyo kuhusiana na kushindwa kulipwa kwa deni hilo.

### 5. Ukiukwaji wa taratibu za Manunuzi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu imegundua kuwa kuna hoja nyingi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo zinatokana na uwepo wa ukiukwaji wa taratibu za uhamishaji wa mali za Serikali kutoka Mamlaka moja kwenda nyengine. Kamati imelibaini hilo katika Shirika la Bandari la Zanzibar ambalo limehamisha umiliki wa LCT Jitihada na kuipeleka Shirika la Meli Zanzibar. Hata hivyo, Shirika halikuweza kuiandikia barua Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kupata ithibati ya uhamishaji wa mali ya umma kwa vile Ofisi hiyo ndio pekee yenye mamlaka ya kutoa ruhusa ya uhamishwaji wa mali za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC inalishauri Shirika la Bandari Zanzibar lifuate ipasavyo taratibu za uhamishaji wa mali ya umma kutoka katika umiliki wao kwenda Shirika la Meli ili kuepusha mkanganyiko wa kumbukumbu za uhifadhi wa mali za Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchunguzi wa hoja nambari 6.1.4.3 inayohusiana na kuwepo kwa Matrekta ambayo hayajafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu. Kamati yetu imebaini kwamba licha ya kuwepo kwa vifaa chakavu katika Taasisi za Serikali na kuhitajika kuuzwa kwa vifaa hivyo, Ofisi ya Msajili wa Hazina hufanya maamuzi ya kufanya mnada wa vifaa vya Serikali bila ya kuzingatia masharti ya kifungu cha 29(a) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Nambari 11 ya mwaka 2016. Hali inayopelekea malalamiko baina ya Taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto hiyo imeikumba Wakala wa Matrekta na Zana za

Kilimo ambapo Watendaji wa Afisi ya Msajili wa Hazina huenda kufanya Mnada bila ya kuushirikisha ipasavyo uongozi wa Wakala. Matokeo yake, kuna baadhi ya matrekta chakavu yamepigwa mnada na kuuzwa kwa bei ndogo ambayo inaweza kupatikana kwa kuuzwa kifaa kimoja au viwili vilivyomo ndani ya trekta lililouzwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imebaini uwepo wa ukiukwaji wa utaratibu wa uuzwaji wa mali chakavu za Wakala unaofanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina ambae hufanya maamuzi ya kuziuza mali zilizoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kabla ya kuthibitishwa. Kwa msingi huo, Kamati inaishauri Ofisi ya Msajili wa Hazina kuchukua hatua za uuzwaji na uondoaji wa mali za umma baada ya kupata maombi ya uuzwaji huo kutoka katika Taasisi husika.

### 6. Taasisi za Serikali kushindwa kufuata maagizo halali ya Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar alibaini uwepo wa hoja nambari 4.3.1.6 kwa Wizara ya Afya inayohusiana na kuwepo kwa Mkataba uliyotolewa kwa Kampuni zilizozuiliwa kutoa huduma Zanzibar (Blacklisted Companies) wenye jumla ya shilingi 4.98. Kamati iliifuatilia kwa karibu hoja hiyo na kugundua kwamba ni kweli kulikuwa na agizo halali la Serikali la kuzuiliwa kwa Kampuni ya Group Six International Limited na Kampuni ya Hainan kutoa huduma zao za ujenzi ndani ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya PAC imechukuwa juhudi ya kuiandikia barua Bodi ya Usajili ya Wakandarasi Zanzibar tarehe 30 Januari, 2024 yenye kumbukumbu nambari CE.81/204/02/36 ili kuweza kujua kama kweli Kampuni hizo zilizuiliwa au zimezuiliwa kufanyakazi Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Lakushangaza, Kamati imebaini kwamba Bodi hiyo haina taarifa yoyote kwamba Kampuni hizo zimezuiliwa kufanya kazi Zanzibar kwani bado

zinaendelea na usajili ambao unatambulika na Bodi hiyo. Hili linathibitisha kwamba baadhi ya Wizara/Taasisi za Serikali hushindwa kuyachukulia hatua ipasavyo maamuzi halali yanayotolewa na Serikali. Ni matumaini ya Kamati kwamba mara tu baada ya kutolewa agizo hilo na Serikali Wizara/Taasisi husika ilitakiwa kuwasilisha ombi maalum kwa Bodi ya Usajili ya Wakandarasi kuhusiana na uzuiaji wa Kampuni hizo kwa maslahi ya umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kwamba Maagizo yanayotolewa na Serikali yanatakiwa yafuatane na utekelezaji wake ili nidhamu ya kazi iweze kupatikana.

**7. Ukiukwaji wa Maamuzi ya Kikao cha Kamati ya Tathmini**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufuatilia ukweli wa hoja nambari 4.3.1.7 inayohusiana na ukiukwaji wa maamuzi ya kikao cha Kamati ya Tathmini. Wizara ya Afya kupitia Kamati yake ya Tathmini ilibariki zabuni ya shilingi bilioni 18.985 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa LOT No. 5, 7, 8 na 10. Hata hivyo, Wizara ya Afya ilishindwa kutekeleza maamuzi ya kikao halali cha Kamati ya Tathmini kwa bei elekezi iliyokubalika badala yake iliamua miradi hiyo itekelezwe kwa gharama ya shilingi bilioni 19.940 jambo ambalo limepelekea ongezeko la shilingi milioni 955.559 ambapo ni kwenda kinyume na kifungu cha 138 (1) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kujua sababu zilizopelekea maamuzi ya Kamati ya Tathmini kushindwa kutekelezwa na Wizara hatimae kuchukua uamuzi wa kuyabadilisha bila ya kufuata utaratibu. Kwa bahati mbaya, Kamati ilielezwa kwamba Wizara ilitaka kuwapa kipaumbele Wazawa kwa kuwasaidia kiuchumi hususan katika utekelezaji wa Miradi ya ndani.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwepo kwa nia njema ya Wizara ya kutaka kuwasaidia Wakandarasi Wazawa kiuchumi. Hata hivyo, taratibu stahiki za kuwawezesha

Wakandarasi hao hazikufuatwa, Kamati ililithibisha hilo kwa kuwataka Watendaji wa Wizara ya Afya kuwasilisha mbele ya Kamati Ripoti ya Kamati ya Tathmini ili kubaini kama kuna sababu au maelekezo hayo lakini kwa bahati mbaya haikuweza kuziona sababu hizo badala yake Wizara iliamua kuchukua hatua za kuwapatia kazi Wakandarasi Wazawa pasi na kufuata utaratibu wa kurudi katika Kamati ya Tathmini.

### 8. Kukosekana kwa hati miliki (title deeds) kwa maeneo yanayotumiwa na Mamlaka ya Maji kwa uzalishaji na usambazaji maji

**Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Ardhi ni Taasisi ya Serikali iliyoundwa na Sheria Namba 6 ya mwaka 2015 ambayo pamoja na mambo mengine inajukumu la kufanya ukaguzi wa maeneo ambayo Taasisi au Watu binafsi wanahitaji kupatiwa hati miliki za Ardhi. Kwa bahati mbaya, utekelezaji wa jukumu hilo umekuwa na changamoto hususan kwa upatikanaji wa hati hizo kwa Taasisi nyingi za Serikali.

**Mheshmiwa Spika,** kuna Taasisi nyingi za Serikali ambazo zimewasilisha maombi yao Kamisheni ya Ardhi lakini zinaendelea kusubiri bila ya maombi yao kupatiwa ufumbuzi. Miongoni mwao ni Mamlaka ya Maji Zanzibar ambayo katika mwaka 2020/2021 imepatiwa hoja ya kutoyapatia hati miliki maeneo yake ya uzalishaji na usambazaji wa maji Unguja na Pemba. Aidha, mwaka 2022/2023 hoja hiyo pia inaweza kujitokeza tena kwa vile utekelezaji wake upo katika asilimia ndogo sana.

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa upande wa Unguja inamiliki maeneo zaidi ya 60 kati ya maeneo hayo ni maeneo 5 tu ndio waliyopata hati miliki (ambayo ni Welezo Matangini, Chuini, Gulioni, Mtoni na Miembeni Madema) na mengine bado hawana hati miliki.

**Mheshimiwa Spika,** kukosekana kwa hati miliki kwa maeneo ambayo Mamlaka ya Maji Zanzibar inayoyatumia kwa ajili shughuli za uzalishaji na usambazaji maji kunaweza

kupelekea migogoro ya ardhi baina ya Mamlaka ya Maji na wananchi wa maeneo husika, uvamizi wa maeneo ambayo yanamilikiwa na Mamlaka ya Maji unaofanywa na wananchi na pia kunaweza kupelekea hasara ya kulipia fidia mara mbili. Aidha, Mamlaka hushindwa kufanya mipango yao ya kimaendeleo katika maeneo hayo pamoja na kuwachukulia hatua za kijinai wale wote wanaoharibu vianzio vya maji vilivyokuwa havina hati miliki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imebaini kuwa ZAWA kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi tayari zimeshakamilisha zoezi la ukaguzi wa maeneo ya vianzio vya maji 32 kwa Mkoa wa Kaskazini na 51 Mkoa wa Kusini Unguja lakini hati miliki za maeneo hayo bado hazijatolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya mawasiliano ya kuiandikia barua Kamisheni ya Ardhi yenye kumbukumbu nambari CE.81/204/02/35 ili Kamati kufahamu ugumu uliopo na kubaini kwamba Kamisheni ya Ardhi bado haijawapatia ZAWA gharama halisi za uandaaji wa hati miliki kwa maeneo waliyokamilisha ukaguzi ya Mkoa wa Kaskazini na Kusini. Lakushangaza zaidi ni kwamba Kamisheni ya Ardhi inaendelea na ukamilishaji wa ukaguzi katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi pamoja na kazi ya upimaji wakati maeneo waliyokamilisha kazi hawajayapatia hati miliki husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inashauri kwamba Kamisheni ya Ardhi iwapatie ZAWA gharama za malipo ya uandaaji wa hati miliki kwa yale maeneo yote yaliyobainika kuwa wanayamiliki kihalali ambayo tayari wameshakamilisha utaratibu wa ukaguzi ili ZAWA iweze kufanya malipo na kupatiwa hati za maeneo yao na kuepukana na changamoto zinazowakabili.

**9. Ajira za muda katika utoaji huduma za ulinzi katika visima vya maji vya ZAWA.**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma haziruhusu uwepo wa ajira za muda katika utoaji wa huduma za umma. Uwepo wa masharti hayo husababisha changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya baadhi ya Taasisi za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Maji Zanzibar, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Taasisi nyengine za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mamlaka ya Maji ZAWA, licha ya Mamlaka hiyo kupata kibali cha uajiri wa Watumishi wa muda 278 wakati wanahitaji Watumishi 394 wa kulinda visima vya maji vipatavyo 400 ambavyo ni roho ya maisha yetu na wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** kama kweli tunataka Mamlaka hii itekeleze majukumu yake kwa ufanisi, ni busara kwa Serikali kuwapatia kibali maalum cha kuongeza uajiri Watumishi wa muda. Hata hivyo, Serikali ihakikishe inafuatilia kwa karibu uajiri huo ili kuepusha kuajiriwa Watumishi wasiokuwa na maadili.

**10. Kutokuteuliwa kwa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Majengo Zanzibar.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya hoja ambazo Mkaguzi anaziibua zinakuwa zinasababishwa katika hatua ya utekelezaji jambo ambalo linapelekea kuwepo kwa hoja nyingi katika Ripoti ya Mkaguzi ambazo zinaweza kuepukika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotembelea Wakala wa Majengo wa Serikali (ZBA) ilibaini kwamba kwa muda mrefu Wakala huo unafanya kazi zake bila ya kuwa na Bodi ya Wakurugenzi. Lakushangaza, Mwenyekiti wa Bodi hiyo tayari ameshateuliwa na Mheshimiwa Rais tangu mwezi 17 Febuari, 2023 takriban mwaka mzima hivi sasa lakini hakuna Mjumbe aliyeteuliwa na Mheshimiwa Waziri hadi Kamati hii inakamilisha kazi

zake katika Wakala huo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokuwepo kwa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Majengo Zanzibar kunapelekea kukwama kwa baadhi ya majukumu ya msingi ya Bodi hiyo na hatimae kuathiri utendaji wa shughuli za Wakala. Kwa mnasaba huo, Kamati yetu inapendekeza kwa Waziri kuchukua juhudi za makusudi kuhakikisha Wajumbe wa Bodi hiyo wanachaguliwa kabla ya muda wa Mwenyekiti kumalizika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia**,** naomba kwa namna ya kipekee kabisa kukushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuwasilisha muhtasari huu wa Ripoti ya Kamati ya PAC kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kazi za Kamati ya PAC zinatekelezwa na Wajumbe wa Kamati kwa usaidizi mkubwa wa Sekretarieti ya Kamati inayojumuisha Makatibu wa Kamati na Wakaguzi kutoka Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hivyo basi kwa heshima kubwa, naomba kutoa shukrani maalum na pongezi za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati ya PAC na Sekretarieti ya Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya bila ya kuchoka wakati wote wa utekelezaji wa majukumu mazito ya Kamati hii hadi tukaweza kuwasilisha Ripoti hii.

**Mheshimwa Spika**, kutokana na umuhimu huo, naomba kuwataja Wajumbe na Sekretarieti hiyo ya Kamati kama ifuatavyo:-

**WAJUMBE WA KAMATI YA PAC**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | MHE. JUMA ALI KHATIB | MWENYEKITI |
| 2. | MHE. MWANAIDI KASSIM MUSSA | MAKAMO MWENYEKITI |
| 3. | MHE. BAKAR HAMAD BAKAR | MJUMBE |
| 4. | MHE. JAMAL KASSIM ALI | MJUMBE |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | MHE. MIRAJ KHAMIS MUSSA | MJUMBE |
| 6. | MHE. SHADYA MOHAMMED SULEIMAN | MJUMBE |
| 7. | MHE. KOMBO MWINYI SHEHE | MJUMBE |
| 8. | MHE. MOHAMED AHMADA SALUM | MJUMBE |

SEKRITARIETI YA KAMATI YA PAC

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Maryam Ali Haji | Katibu wa Kamati |
| 2. | Ndg. Said Khamis Ramadhan | Katibu wa Kamati |
| 3. | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu wa Kamati |
| 4. | Ndg. Adam Maulid Simai | Katibu wa Kamati |
| 5. | Ndg. Robert Laurian Mweiro | Mkurugenzi Tehama - Afisi ya Mdhibiti |
| 6. | Ndg. Ramadhan Iddi Hassan | Mkurugenzi Wa Ukaguzi - Afisi ya Mdhibiti |
| 7. | Ndg. Nassor Mdachi Mwinyi | Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Unguja) |
| 8. | Ndg. Juma Mohammed Juma | Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Mifumo) |
| 9. | Ndg. Mussa Kadir Mussa | Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Mifumo) |
| 10. | Ndg. Shehe Abdallah Ali | Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Unguja) |
| 11. | Ndg. Maryam Ali Khamis | Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Mifumo) |
| 12. | Ndg. Mariyam Alhaji Juma | Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Unguja) |
| 13. | Ndg. Moh'd Suleiman Amour | Mkaguzi - Afisi ya Mdhibiti (Pemba) |

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti hii imeeleza kwa ufupi yale ambayo yamebainika katika kazi za Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Utekelezaji zaidi wa kazi iliyofanyika unapatikana katika Ripoti halisi ya Kamati yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe mmetumiwa katika vishkwambi vyenu na Afisi yetu ya Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako

Tukufu kwa kunisikiliza na ninawaomba waijadili na hatimae kuipitisha Ripoti hii ya Kamati ya PAC kwa lengo la kupata majibu ya utekelezaji wa Serikali ifikapo mwezi wa Septemba kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 109(17) ya Baraza la Wawakilishi ili kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa mapato na matumizi ya rasilimali za Umma kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

……………….
Juma Ali Khatib,
Mwenyekiti,
Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali,
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
<u>ZANZIBAR.</u>